JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

**WAKALA WA USAJILI UFILISI NA UDHAMINI (RITA)**

# MAADHIMISHO YA SIKU YA USAJILI WA MATUKIO MUHIMU YA BINADAMU NA TAKWIMU

## (CRVS DAY) AGOSTI 10, 2018



Waziri wa Katiba na Sheria
**Mhe. Prof. Palamagamba Kabudi**

### MAELEZO YA WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA MHE. PROF. PALAMAGAMBA KABUDI KUHUSU MAADHIMISHO YA SIKU YA USAJILI WA MATUKIO MUHIMU YA BINADAMU YA TAKWIMU

Leo tarehe 10 Agosti ni Siku ya Usajili wa Matukio muhimu ya binadamu na Takwimu ambapo kwa mara ya kwanza inaadhimishwa hapa nchini na kauli mbiu ya mwaka huu ni ***"Kuhamasisha ubunifu katika Mfumo wa Usajili wa Matukio Muhimu na Takwimu kwa ajili ya utawala na maisha bora .***

Kwa miaka kadhaa kumekuwa na juhudi mbalimbali za kuleta maboresho katika mifumo ya Usajili wa matukio muhimu ya Binadamu. Mkutano wa kwanza wa Mawaziri wenye dhamana ya Usajili wa Matukio Muhimu ya Binadamu uliofanyika Addis Ababa, Ethiopia mwaka 2010, uliamua kuanzisha ushirikiano na kuunganisha juhudi za kuboresha mpango wa mfumo wa Usajili wa matukio muhimu ya binadamu na Takwimu barani Afrika.

Tangu uamuzi huo upitishwe, Mawaziri tumekuwa tukikutana kila baada ya miaka miwili, suala linaloonyesha utashi wa hali ya juu wa kisiasa wa nchi za Afrika. Tulipokutana katika mkutano wa Nne tulipendekeza na kukubaliana Tarehe 10 Agosti ya kila mwaka kuwa ni Siku ya Kuadhimisha Usajili wa Matukio Muhimu ya Binadamu na Takwimu barani Afrika. Baraza Kuu la Umoja wa Afrika (AU) katika Kikao chake cha kawaida cha 32 kilichowakutanisha Wakuu wa Nchi, kilichofanyika Januari 25-26, 2018, lilipitisha mapendekezo hayo yaliyotolewa na tamko la mkutano wa mawaziri.

Hapa nchini juhudi za kuimarisha mfumo wa Usajili zilianza mnamo mwaka 2013 kwa kubuni Mkakati wa kitaifa wa Usajili wa Matukio Muhimu ya Binadamu na Takwimu *(National Civil Registration and Vital Statistics Strategy)* ambao umeanza kutekelezwa na kupata mafanikio chanya kupitia mipango mbalimbali iliyogawanyika kutokana na makundi ya umri. Ili kuimarisha mfumo wa Usajili, Serikali imeanza kuzifanyia mapitio sheria zinazoongoza usajili wa matukio ili kuja na mapendekezo ya kuzirekebisha ziendane na wakati na zikidhi mahitaji ya usajili yaliyopo sasa.

**KWA NINI TUNAADHIMISHA CRVS DAY?**
Tanzania pamoja na nchi nyingi za bara la Afrika kwa takribani miongo kadhaa, tumekuwa na mifumo ya Usajili wa matukio muhimu, lakini mingi ya mifumo hiyo haikuwa ya lazima kisheria, haikushirikisha maeneo yote na haikukidhi vigezo.

Matumizi ya Teknolojia ya kisasa ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) katika mfumo wa usajili katika nchi nyingi barani Afrika ni duni. Katika nchi zinazotumia TEHAMA mfumo wa usajili bado haijaunganishwa na mifumo mingine ya Serikali kama vile, Takwimu za Taifa, Huduma za Afya, Vitambulisho vya Taifa na Huduma za Uchaguzi. Tayari Nchi yetu tumeanza kuimarisha matumizi ya TEHAMA katika mifumo ya usajili ambayo imeanza kuunganishwa na mifumo mingine ya usajili na utambuzi nchini.

Lengo la kuadhimisha Siku ya Usajili wa Matukio Muhimu ya Binadamu Agosti 10 ya kila mwaka barani Afrika ni kuelimisha Umma juu ya umuhimu wa kila mtu kutambulika barani Afrika, kwa kutumia mfumo wa usajili unaofanya kazi kwa ufanisi na ambao unakidhi, kuwahusisha na kuwajumuisha watu wote.

**CRVS KWA AJILI YA UTAWALA BORA NA MAISHA BORA**
Usajili wa Matukio Muhimu ya Binadamu na Takwimu ni suala la msingi katika mifumo ya kisiasa na ya utawala bora na inasaidia kujumuisha jamii katika maamuzi, kulinda haki za binadamu, kuhakikisha huduma za jamii muhimu zinawafikia walengwa na pia kutatua changamoto za ubaguzi na kuleta uwiano sawa katika masuala ya maendeleo ya kiuchumi na kijamii.

Daftari la Usajili wa Matukio muhimu ya Binadamu linawawezesha watu kupata nyaraka muhimu za kisheria zinazoweza kulinda haki zao za msingi na haki za binadamu kama kuwa na jina, kitambulisho, uraia, haki za mwananchi na huduma za msingi za wananchi.

Cheti cha kuzaliwa, ni nyaraka muhimu ya kisheria ambayo ni ushahidi wa kuonyesha umri wa mtu na husaidia kuzuia uvunjifu wa haki za watoto ikiwamo ajira za watoto, usafirishaji haramu wa watoto na matumizi ya watoto katika vita hasa katika wakati wa hali ya hatari. Vilevile, Uthibitisho wa umri ni taarifa inayohitajika ili kuweza kupata huduma nyingine nyingi za msingi kama kupata kazi, kupata nafasi za masomo, kupata mikopo ya elimu, n.k

Takwimu za usajili wa matukio muhimu ya binadamu zinasasaidia kupata taarifa sahihi za wingi wa watu zinazoainisha umri, jinsia na maeneo ya kijiografia yaliyo katika hatari ya kuachwa nyuma katika mchakato wa maendeleo ya Taifa. Takwimu hizi ni muhimu sana kwa taifa letu ambalo kwa sasa inafanya juhudi za kujenga uchumi wa viwanda ambao utaiwezesha nchi kuwa katika uchumi wa kati kufikia mwaka 2025. Pia ni muhimu katika kupanga programu za chanjo za watoto, huduma za afya, Shule za Awali na Shule za Msingi.

Takwimu za usajili wa vifo zinatoa ushahidi wa sababu zinazosababisha vifo vingi hususani maradhi na husaidia katika kupanga udhibiti wa matatizo ya maradhi hayo na kiafya. Takwimu hizo pia husaidia kuboresha Huduma za Afya na Jamii kwa ajili ya maisha bora.

Aidha, takwimu za ndoa na kuvunjika kwa ndoa ni muhimu katika kufahamu miundo ya kifamilia na sheria za kuvunjika kwa ndoa ndani ya kila nchi husika na pia zinasaidia kupanga programu za huduma za kifamilia na jamii na kulinda haki za wanawake na watoto.

**KUHAMASISHA UBUNIFU WA MBINU ZA KUBORESHA MFUMO WA USAJILI WA MATUKIO MUHIMU YA BINADAMU**
Matumizi ya teknolojia katika kutoa huduma bora, zenye uhakika na sahihi katika mfumo wa Usajili wa Matukio Muhimu ya Binadamu na Takwimu Muhimu (CRVS) ni muhimu sana kwa Bara la Afrika, ambalo hali ya usajili sio ya kuridhisha na hutumia mifumo duni ya kuweka kutuma na kutunza takwimu.

Serekali ya Tanzania kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo tumeanza uwekezaji katika ubunifu wa kupata teknolojia sahihi na ya gharama nafuu, utakaowezesha kuleta ushirikiano katika kuunganisha takwimu na taarifa, usimamizi mzuri wa taarifa, usiri na mfumo bora wa kuhakiki taarifa barani Afrika. Kupitia Mpango wa Usajili wa Watoto wa Umri Chini ya Miaka Mitano tumebuni mfumo ambao simu za mkononi hutumika kutuma taarifa za watoto waliosajiliwa kwenda kwenye kanzidata ya Wakala. Vilevile tumeweka vifaa vya kisasa vilivyo na uwezo wa kutunza taarifa nyingi kwa wakati mmoja.



**Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Kassim Majaliwa (Mb) akikabidhi cheti cha kuzaliwa cha mtoto aliyesajiliwa kupitia Mfumo mpya wa Usajili katika Viwanja vya Nyerere jijini Dodoma.**

Bila ya kuwa na mfumo unaowezesha upatikanaji wa taarifa za uhakika, zikiwemo taarifa za sababu za vifo, kutoka katika mfumo unaofanya kazi kwa uhakika wa maeneo yote ya Usajili wa Matukio Muhimu, malengo ya maendeleo ya taifa, ukanda na dunia hayawezi kufanyiwa tathmini na kufuatiliwa kwa karibu.

Napenda kuwashukuru wadau wote wa maendeleo ambao tunashirikiana nao katika kuhakikisha kwamba nchi inapata mfumo bora na madhubuti wa usajili. Wadau hao ni pamoja na Benki ya Dunia, Shirika la Afya Duniani, Serikali ya Kanada, Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumuia Watoto (UNICEF), Bloomberg Data for Health, Centre for Desease Control (CDC) Kampuni ya Simu za Mkononi ya Tigo. Vilevile, shukrani ziende kwa Wizara, taasisi na Idara za Serikali ambazo zimekuwa sehemu ya mafanikio ya hatua iliyofikiwa ya utekelezaji wa Mkakati wa Usajili wa Matukio Muhimu ya Binadamu na Takwimu.

Ni imani yangu kwamba maadhimisho haya ya Siku ya Usajili wa Matukio Muhimu ya Binadamu yatawawezesha wananchi wengi kupata elimu kuhusu usajili wa matukio haya mara tu yanapotokea

Mhe. Profesa Palamagamba Kabudi
**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA**